Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
**Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia**

# ELIMU *Bulletin*

JARIDA LA MTANDAONI: *Toleo Na.25 - 2023*

wizara_elimuTanzania wizara_elimuTz www.facebook/moestvt.com www.wyestu.blogspot.com www.moe.go.tz ELIMUTZ

*Tunaboresha Elimu Yetu*






# Rais Samia akutana na kufanya mazungumzo na Viongozi, Wawakilishi TAHLISO na ZAHILFE

## - KAZI IENDELEE -




## BODI YA UHARIRI

Dkt. Lyabwene M. Mtahabwa
***Kamishna wa Elimu***

Atupele Mwambene
***Mkurugenzi wa Sera na Mipango***

Sylvia Lupembe
***Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini***

Nelly Mtema
***Mhariri Msaidizi na Mwandishi TSN***

**Wachangiaji:**
Oliva Kato
Elizabeth Pancras
Ipyana Mwaipaja

**Mawasiliano:**
Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia,
Mji wa Serikali Mtumba, Mtaa wa Afya - Dodoma
S.L.P. 10, 40479 DODOMA.
Simu: +255 26 296 3533

**Jarida hili linatolewa na**
Kitengo cha Mawasiliano Serikalini
Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

# TAHARIRI

## Serikali imeendelea kuongeza Fursa za Upatikanaji wa Elimu na Mafunzo katika Vyuo vya Ufundi Stadi (VETA)

Kwa muda mrefu kiu ya wananchi imekuwa ni kuona elimu ujuzi inakuwa kitovu cha elimu yetu hapa nchini. Katika kufikia hilo Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia inafanya mambo mengi ikiwemo mapitio ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 na maboresho ya Mitaala ya Elimu ambayo yanalenga kuwezesha elimu ujuzi kufundishwa katika shule, Vyuo vya Kati vya ufundi na Vyuo Vikuu.

Vyuo vya ufundi stadi (VETA) ni miongoni mwa vyuo vya kati ambavyo vitakuwa chachu na nguzo kuu katika kuhakikisha elimu ujuzi inatolewa na kuwafikia vijana wengi zaidi nchini lengo likiwa ni kuongeza idadi ya wataalamu na kuhakikisha vijana wa Kitanzania wanapata elimu, ujuzi, maarifa na stadi zitakazowawezesha kuingia katika soko la ajira kwa kuajiriwa, kujiajiri ama kuajiri.

Katika kutambua hilo Serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kushirikiana na wadau imeendelea kuongeza fursa za upatikanaji wa elimu na mafunzo katika Vyuo vya VETA kupitia ujenzi, upanuzi na ukarabati wa majengo na miundombinu ya vyuo hivi.

Kupitia Mradi wa Kukuza Ujuzi na Stadi za Kazi (Education and Skills for Productive Jobs -ESPJ) ambao umetekelezwa na Wizara, takribani bilioni 39 zilitolewa kwa Halmashauri na Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) Makao Makuu kwa ajili ya kuwezesha ujenzi, upanuzi na ukarabati wa vyuo vya ufundi Stadi 39 ambapo Halmashauri nne za Kongwa, Kasulu, Nyasa na Ruangwa tayari zimeshakamilisha ujenzi na vyuo vinaendelea kutoa mafunzo.

Aidha, VETA Makao Makuu ilikuwa na jukumu la kusimamia na kujenga vyuo vya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi katika Wilaya 25 ambao kwa kiwango kikubwa umekamilika na tayari baadhi ya vyuo vimeanza kutoa mafunzo.

Mbali na ujenzi huo wa Vyuo vya VETA vya Wilaya, Serikali pia imejenga vyuo vya VETA vya mikoa ambapo mpaka sasa ni Mkoa wa Songwe pekee ambao haujajengewa chuo cha VETA, lakini kupitia Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda ni kwamba fedha za kujenga Chuo katika mkoa huo tayari zimetengwa na ujenzi utaanza karibuni.

Katika bajeti ya Mwaka 2022/23 Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imetenga Shilingi bilioni 100 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa vyuo vya ufundi na mafunzo ya Ufundi stadi katika Wilaya 63 ambazo bado hazina vyuo hivyo, ili kufanya Wilaya zote nchini kuwa na vyuo VETA.


Kongole kwa Wilaya zote ambazo zimeonesha utayari wa kupokea mradi wa ujenzi wa vyuo vya VETA kwa kutenga ardhi, hii inaonyesha nia ya viongozi wa Wilaya hizo kuona vijana katika maeneo yao wanapata ujuzi, maarifa na stadi zitakazowawezesha kujenga uchumi wa Taifa.

Waziri Mkenda ana kauli yake pendwa inayosema "Katika Elimu, yajayo yanafuraisha," nasi tunasema "Katika Jarida hili kuhusu VETA yajayo yanafurahisha."



*Muonekano wa majengo ya Chuo cha VETA Mbarali*

Uwezeshaji Wanafunzi Elimu ya Juu >



# Rais Samia akutana na kufanya mazungumzo na viongozi na wawakilishi TAHLISO, ZAHILFE

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan ameelekeza Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kupandisha posho ya kujikimu ya wanafunzi wa elimu ya juu hadi kufikia Sh. Elfu kumi kwa siku.

Rais Samia amesema hayo jijini Dodoma wakati akizungumza na wawakilishi wa Jumuiya za Wanafunzi wa Taasisi za Elimu ya Juu Tanzania TAHLISO na ZAHILFE katika viwanja vya Ikulu Chamwino jijini Dodoma.

Aidha amesema Serikali inafanya jitihada mbalimbali za kuinua elimu ya juu kwa kuongeza fursa za upatikanaji wake ikiwemo kuongeza wigo wa mikopo na kuwataka kuhakikisha wanarejesha mikopo hiyo ili iwanufaishe na wengine.

"Labda niwaambie tumekamilisha mkataba na Benki ya NMB wa thamani ya Sh. Bilioni 200 ili wazazi ambao mishahara yao inapita benki waweze kukopa kwa ajili ya vijana wao," amesema Rais Samia.

Dkt. Samia amewataka wanafunzi kuwa na ufahamu kuhusu mwelekeo wa nchi na aina ya Taifa tunalotaka kulijenga ambalo litajitegemea kiuchumi huku akiwasisitiza kuweka mkazo katika masomo na kujiepusha na vitendo viovu.

Mhe. Samia ameupongeza uongozi wa Wizara ya Elimu kwa namna unavyotekeleza majukumu yake kwa ufanisi na kwa wakati.

"Nitumie fursa hii kumshukuru sana Mhe. Prof. Adolf Mkenda, Katibu Mkuu na Timu yote ya Wizara kwa kazi nzuri sana mnayoifanya kuwahudumia watoto hawa na mipango mingi ambayo nimeiagiza Prof. Mkenda na timu yake wameibeba na kwenda kuitekeleza vizuri sana tena kwa muda mfupi. Zamani ilizoeleka unaagiza inakwenda kutekelezeka kwa muda mrefu ukiuliza unaambiwa fedha lakini sasa hivi ukiagiza linafanyika, tunasonga mbele," amesema Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Kwa upande wake Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Mhe. Prof. Adolf Mkenda amemshukuru Rais Samia kwa kutoa fursa ya kukutana na Wawakilishi hao na kumshukuru kwa kutoa kipaumbele katika sekta ya elimu ambapo alipoingia madarakani ameongeza mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu kutoka TZS bilioni 464 hadi kufikia bilioni 654.

Mkenda ameongeza kuwa Wizara iliunda Kamati kwa lengo la kuangalia mfumo wa utoaji mikopo hususan kuangalia vigezo vitakavyoweza kutumika kuhahakisha mikopo inawafikia walengwa. Aidha amesema katika kuongeza wigo wa ugharamiaji elimu ya juu kupitia ufadhili wa Samia Scholarship wanafunzi 640 wanaosoma fani za Sayansi wamepata ufadhili katika Mwaka wa fedha 2022/23.

Katika hatua nyingine Mkenda amemuahidi Rais kuwa Wizara na Taasisi zinazosimamia Elimu ya kati na ya Juu zitaongeza ushirikishwaji wa serikali za wanafunzi kwa kuweka mfumo utakaorahisisha mawasiliano na viongozi hao.

"Mhe. Rais kwa kuanzia tumeteua mjumbe mmoja kupitia uongozi wa TAHLISO kuingia kwenye Bodi ya Mikopo ya Elimu ya juu (TCU). Tumeangalia kwa TCU sheria hairuhusu lakini wamesema wako tayari kuingiza mjumbe mmoja mwanafunzi katika baadhi ya vikao vyao ili kupitia huu ushirikishwaji changamoto ziweze kufikishwa na kutatuliwa kwa wakati," amesema Prof. Mkenda.

Kwa upande wake rais wa TAHLISO, Frank Nkinda amempongeza Rais Samia kwa kuendelea kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia kwenye Vyuo ya elimu ya juu kupitia Mradi wa HEET pamoja na kuondoa asilimia 6 ya tozo ya kutunza thamani ya fedha na asilimia 10 ya kuchelewa kurejesha mikopo.

Nkinda ameshukuru na kupongeza ushirikiano wanaopata kutoka Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU), Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTVET).

Miundombinu Kukuza Ajira >

# Majaliwa atoa wito waajiri nchini kushirikiana na Serikali kukuza ujuzi ili kuongeza soko la ajira




Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa ametoa wito kwa waajiri nchini kuendelea kushirikiana na Serikali kuhakikisha malengo ya kukuza ujuzi na kuongeza soko la ajira yanafanikiwa kwa mustakabali wa Taifa.

Wito huo umetolewa jijini Dar es Salaam wakati wa hafla ya kuwatambua na kuwapongeza waajiri na wadau wanaoshirikiana na Serikali katika kukuza na kuendeleza ujuzi kwa wanafunzi walioko vyuoni na waliohitimu.

Amesema maendeleo ya uchumi wa nchi yoyote yanategemea nguvu kazi yenye ujuzi hivyo mchango wa wadau kama waajiri ni muhimu katika kufanikisha hilo.

"Niwapongeze waajiri kwa ushiriki wenu katika kutoa nafasi za mafunzo kwa vitendo, hii ni pamoja na uanagenzi. Aidha nawapongeza kwa ushiriki wenu katika katika kuaandaa mitaala inayotumika katika Vyuo na Taasisi za Elimu ya Ufundi na mafunzo ya Ufundi Stadi", amesema Mhe. Majaliwa.

Ameongeza Serikali inatambua na inathamini juhudi zinazofanywa na waajiri hao katika kuliwezesha Taifa kukabiliana na changamoto ya ajira na kuiwezesha nchi kuwa na rasilimaliwatu yenye ujuzi.

"Niwahakikishie waajiri Serikali inathamini mchango wenu katika kuliwezesha taifa kukabiliana na changamoto ya ajira. Kazi mnayoifanya imedhihirisha uzalendo wa hali ya juu na inaonesha wazi kuwa waajiri mnaunga mkono juhudi za Serikali katika kuhakikisha Tanzania inakuwa nchi yenye rasilimaliwatu wenye ujuzi unaokidhi mahitaji ya soko la ajira na kujenga uchumi imara katika nchi,"ameongeza Waziri Mkuu Majaliwa.

Kwa upande wake Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Adolf Mkenda amemweleza Waziri Mkuu kuwa Wizara itaendelea kusimamia Mkakati wa Taifa wa uendelezaji wa ujuzi 2016/17 -2025/26 ambao moja ya malengo yake ni kuwa na ushirikiano kati ya waajiri wadau na vyuo au taasisi za elimu.

"Tumekamilisha tracer study ya kutambua hali ya ajira kwa wahitimu wa vyuo vyetu vya ufundi iwapo wameajiriwa uwezo wao wa kazi na mapungufu.Hii itasaidia kuboresha mitaala yetu na hatimaye kuboresha elimu itolewayo,"amesema Prof. Mkenda.

Naye Katibu Mtendaji Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi Dkt. Adolf Rutayuga amesema mafunzo yanayotolewa kwenye vyuo na Taasisi za elimu na mafunzo ya ufundi stadi yanaongozwa na mahitaji ya soko la ajira hivyo kukutana na waajiri ni fursa nzuri katika kukumbushana nafasi yao katika kukuza ujuzi nchini.

Kauli mbiu ya hafla ya kuwatambua na kuwapongeza waajiri na wadau wanaoshirikiana na Serikali katika kukuza na kuendeleza ujuzi kwa wanafunzi walioko vyuoni na waliohitimu kwa mwaka 2023 ilikuwa Kuimarisha Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi kwa uzalishaji wa wafanyakazi wenye ujuzi nchini Tanzania.

Uimarishaji TEHAMA >



# Chuo cha Teknolojia cha India kuanzishwa nchini Tanzania

Serikali ya India inatarajia kuazisha Chuo cha Teknolojia (Indian Institute of Technology) nchini Tanzania ambacho kitakuwa kinatoa kozi ya masuala ya Tehama na kozi nyingine zinazoendana na mlengo huo.

Akizungumza jijini Dar es Salaam mara baada ya kuongea na timu kutoka Chuo hicho Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Mhe. Prof. Adolf Mkenda amesema Serikali ya Tanzania itashirikiana na nchi hiyo ili lengo la kuanzisha Chuo hicho liweze kutimia.

Amesema kwa kuwa Chuo cha Teknolojia cha India kimepiga hatua ya juu zaidi katika masuala ya Teknolojia hivyo ujio wa ujumbe huo ni hatua ya kuona mazingira ya nchini kwetu katika kutimiza adhma yao ya kuanzisha chuo hapa nchini.

"Wenzetu hawa wanataka kuanzisha Chuo hapa nchini tuliwaalika waje na tayari wamefanya mazungumzo na Serikali ya mapinduzi ya Zanzibar na kuahidiwa ardhi kwa ajili ya kuazisha huko, lakini kwa kuwa suala la elimu ya juu ni la muungano tunaangalia taratibu za urekebu kuona nini kinaweza kufanyika ili kazi hii iweze kuanza,"amesema

"Wanataka kuanza kuchukua wanafunzi mwezi Oktoba mwaka huu ni muda mfupi sana kutokea sasa ila tutafanya kazi usiku na mchana kuona ni nini kinaweza kufanyika tukasonga mbele,"amesema

Waziri Mkenda Amesema pia timu hiyo kutoka India imekwenda kutembelea Chuo Kikuu cha Afrika cha Nelson Mandela kilichoko jijini Arusha pamoja na Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT) ili kuona vifaa vya kujifunzia na kufundishia vilivyopo na namna ambavyo wanaweza kufanya kazi kwa pamoja.

"Timu hii tutakutana nayo tena Februari 17 mwaka huu ili kwa pamoja tuangalie rasimu ya makuballiano (MOU) ili tuone tunakwendaje," alisema Waziri Mkenda

Kwa upande wake Balozi wa India nchini Tanzania Binaya Pradhan Serikali ya India imejizatiti (committed) kufanya kazi na Serikali ya Tanzania ili kuhakikisha pamoja na mabo mengine lengo la kuanzia Chuo nchini Tanzania linafanikiwa.

Udhibiti Ubora wa Elimu >

# Vitabu 16 vyapigwa marufuku kutumika shuleni, Taasisi za Elimu

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imepiga marufuku matumizi ya vitabu 16 vinavyokwenda kinyume na maadili kwenye Shule na Taasisi zote za Elimu.

Vitabu hivyo vimepigwa marufuku na Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Mhe. Prof. Adolf Mkenda kwa mamlaka aliyopewa chini ya Kifungu cha 59 cha Sheria ya Elimu Sura ya 353.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dodoma Prof. Mkenda amesema kama taifa tuna mila na desturi za kufuata na katika kufundisha na kulea watoto na kwamba shule zina wajibu wa kuendana na taratibu hizo katika kuwaandaa watoto.

"Nahimiza wazazi mkague mabegi ya wanafunzi kuhakikisha vitabu hivi havitumiki nyumbani; ukaguzi na ufuatiliaji huu ni endelevu ili kubaini kama vitabu kama hivi hipo katika shule tuweze kichukua hatua,"amesema Profesa Mkenda

Amevitaja vitabu hivyo kuwa ni Diary of a Wimpy Kid, Diary of a Wimpy Kid -Rodrick Rules, Diary of Wimpy Kid - The Last Straw, Diary of Wimpy Kid-Dog Days, Diary of a Wimpy Kid The Ugly Truth, Diary of a Wimpy Kid -Cabin Fever, Diary of a Wimpy Kid - The Third Wheel na Diary of a Wimpy Kid - Hard Luck.

Vingine ni Diary of a Wimpy Kid - The Long Haul, Diary of a Wimpy Kid -Old School, Diary of a Wimpy Kid -Double Down, Diary of a Wimpy Kid-The Gateway, Diary, Diary of a Wimpy Kid-Diper Overlode, Is for TANSGENDER ( you know best who you are!), Is for LGBTQIA ( find the words that make you you) na Sex Education a Guide to life.

Prof. Mkenda ametoa rai kwa watanzania kupiga namba 0262160270 ya mezani na 0737 962965 ya mkononi ili kutoa taarifa ya uwepo wa vitabu hivyo shuleni na kwamba hatua kali zitachukuliwa kwa shule yoyote itakayokutwa na vitabu hivyo ikiwemo kufutiwa usajili.



Udhibiti Udanganyifu Mitihani >



# Chunguzeni udanganyifu mtihani Kidato cha Nne - Prof. Mkenda

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Mhe. Profesa Adolf Mkenda amemuagiza Kamishna wa Elimu kufanya uchunguzi wa kina kwa Shule nne zilizobainika kufanya udanganyifu mkubwa katika mtihani wa kidato cha nne mwaka 2022.

Prof. Mkenda amesema hayo alipokutana na Wazazi na walezi wa Wanafunzi waliofutiwa matokeo ya Mtihani wa Kidato nne 2022 wa Shule ya Sekondari Thaqaafa ya Jijini Mwanza kwa ajili ya kuwasikiliza.

Amezitaja shule hizo kuwa ni Cornelius ya Kinondoni Dar es Salaam, Thaqaafa ya Mwanza, Mnemonic ya Zanzibar na Twibhoki iliyoko Mara na kumtaka Kamishna huyo kuchukua hatua kali kulingana na ripoti ya uchunguzi huo.

Mkenda amesisitiza wazazi kuwalea watoto katika maadili ili watambue kuwa udanganyifu si mzuri na una madhara makubwa katika upande wa haki, maadili na uweledi. "Tunapowapeleka watoto shule tunataka wajifunze waelewe ili baadae waje watumikie taifa. Sasa mtu anakuja kuwa daktari au mhandisi au rubani kwa kuiba mtihani, madhara yake ni makubwa sana," ameongeza Mkenda.

Mkenda amewapa pole wazazi na kuwataarifu kuwa mitihani hiyo imefutwa na hivyo kilichopo ni kurudia mitihani.

"Kuhusu kurudia mtihani tumewasikiliza maombi yenu, ninashukuru kuwa hamna anayesema ameonewa sote tunakubaliana kuwa kulikuwa na udanganyifu na hivyo niseme matokeo yamefutwa na kikubwa ni maombi ya kurudia mtihani. Hili tunalichukua tutawasiliana nanyi baada ya kulifanyia kazi kwani ni suala la kibajeti pia," amefafanua Mkenda.

Naye Adam Malima, Mkuu wa Mkoa wa Mwanza akiwa katika kikao hicho amesema Serikali haitalea shule zinazofanya udanganyifu wa mitihani na kuongeza kuwa wanafunzi wanatakiwa wapimwe kwa uwezo na sio kwa kudanganya.

Katika maelezo yao yaliyotolewa kupitia Mwenyekiti wa wazazi hao, Patrick Msagati wameomba Serikali kuwahurumia na kuruhusu matokeo kuachiliwa au kuwapa nafasi ya kurudia mtihani.

"Tunaomba Serikali ichukue hatua kali kwa shule kama hizi kwani zimetusababishia madhara makubwa sisi kama wazazi na watoto pia. Ikiwezekana shule hizi zifungiwe," amesema Michael Zayumba, mmoja wa wazazi.

Matumizi Nishati Mbadala Vyuoni >

# Prof. Mdoe avitaka Vyuo vya Ualimu kutumia Nishati Mbadala kupikia vyakula

Vyuo ya ualimu vya umma vimetakiwa kuhama kutoka kwenye matumizi ya kupikia kuni na mkaa kwenda kwenye matumizi ya nishati mbadala ikiwemo jua, gesi, bayogesi na mkaa poa.

Hayo yamesemwa leo wilayani Mpwapwa na Kaimu Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. James Mdoe wakati akifungua rasmi mafunzo ya utunzaji mazingira endelevu na ujanishaji kwa wakufunzi na Menejimenti za vyuo vya ualimu vya umma yanayoratibiwa na Wizara kupitia Mradi wa Kuendeleza Elimu ya Ualimu (TESP).

Amesema Serikali inatambua umuhimu wa utunzaji mazingira na katika kuhakikisha hilo imeweka mikakati mbalimbali ya kudhibiti uharibifu wa mazingira ikiwemo kulinda vyanzo vya maji, kupunguza matumizi ya hewa ya ukaa, kutokata miti hovyo na kupunguza matumizi ya nishati zitokanazo na miti kama kuni na mkaa.





"Ni matarajio ya Wizara kuwa baada ya mafunzo haya mtajiwekea mikakati na mpangokazi wa utekelezaji wa yote mliyojifunza ili kufikia malengo tuliyojiwekea ili kupunguza gharama za uendeshaji katika vyuo vyetu" amesema Prof. Mdoe.

Prof. Mdoe amevitaka vyuo hivyo kuweka kipaumbele kwenye uvunaji wa maji ya mvua, kupunguza matumizi holela ya maji, kuweka taa za umeme zenye kutumia nishati ndogo na kuhimiza elimu ya 3Rs (Reuse, Reduce and Recycle).

"Vilevile mkaweke mikakati thabiti ya kuteketeza taka ngumu kwa kuzingatia miongozo ya mamlaka zenye dhamana ya mazingira na usalama wa afya. Juhudi hizo ziende sambamba na upandaji miti, maua na utunzaji wa mazingira," amesema Prof. Mdoe.

Naye Mkurugenzi Msaidizi wa Elimu ya Ualimu, Huruma Mageni amesema lengo la mafunzo hayo ni kuhakikisha kuwa kuna mkakati thabiti wa utunzaji wa mazingira endelevu na ujanishaji pamoja na kuboresha utunzaji wa mandhari na mazingira asili.

"Mafunzo haya yanajumuisha Wakuu wa vyuo vya ualimu vyote 35 vya umma na wakufunzi wanne kutoka kila chuo na hivyo kufanya jumla ya washiriki kuwa 175 ambao watakuwa na jukumu la kusimamia masuala ya mazingira katika vyuo vyao," ameongeza Mageni.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Wakuu wa Vyuo vya Ualimu Taifa, Augustino sahili ambaye pia ni mshiriki wa mafunzo hayo ameishukuru Wizara kwa kuandaa mafunzo hayo muhimu na kuahidi kwenda kutekeleza kwa vitendo wafikapo vyuoni kwao.

"Mafunzo haya ni muhimu na yana tija kwani yataenda kubadili mitizamo yetu juu ya utunzaji mazingira na ujanishaji na hivyo kuwezesha vyuo vyetu kupunguza gharama za uendeshaji," amesema Sahili.

# Maelekezo Kuboresha Elimu >



## Jikiteni kufundisha Kilimo, Prof. Mkenda akiambia chuo cha MJNUAT



Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Mhe. Prof. Adolf Mkenda amekitaka Chuo Kikuu cha Mwalimu Julius K. Nyerere cha Kilimo na Teknolojia (MJNUAT) kilichopo Butiama mkoani Mara kujikita kutoa mafunzo kwenye eneo la kilimo kwa upana wake ambao ndio msingi halisi wa uanzishwaji wa chuo hicho.

Prof. Mkenda ameyasema hayo Wilayani Butiama alipotembelea chuo hicho na kuwataka kuhakikisha kuwa pamoja na mafunzo wanafanya tafiti na kusambaza matokeo ya tafiti hizo ili kunufaisha wakulima kwa kuongeza tija na uzalishaji.

Waziri Mkenda ameeleza kuwa chuo hicho kitaanza rasmi kutoa mafunzo mwaka huu 2023 na kuagiza uongozi wa chuo kuhakikisha matayarisho yote yanakamilika.

Amesema mikakati mbalimbali itatumika kuhakikisha wanafikia vigezo vya kupata ithibati ili kuruhusu kutoa mafunzo ikiwemo kuongeza wanataaluma na kuweka mazingira na miundombinu stahiki ya kufundishia na kujifunzia.

"Tutahakikisha MJNUAT Butiama kinaanza kutoa Mafunzo mwaka huu 2023, tayari Serikali imetoa Shilingi bilioni 2.6 kwa ajili ya kukarabati majengo yaliyopo na kujenga hosteli mpya 2 ili wanafunzi watakapoingia wakae katika mazingira bora," amefafanua Waziri Mkenda.

Profesa Mkenda ameongeza kuwa Serikali pia imetenga kiasi cha Shilingi bilioni 102 kupitia Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi (HEET) kwa ajili ya kujenga makao makuu ya Chuo hicho hapo hapo Butiama.

Amesisitiza kuwa uwepo wa MJNUAT ni moja ya njia za kuenzi maono ya Baba wa Taifa kuhusu kutoa elimu ujuzi ikiwemo elimu ya kilimo.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Butiama, Mhe. Mosses Kaegele ameishukuru Serikali kwa kuendeleza Ujenzi wa Chuo Kikuu cha MJNUAT na kuhakikisha kinakwenda kuanza kutoa mafunzo mwaka huu.

"Tunapongeza sana kwa hatua hii ya Wizara kuhakikisha Chuo kinaanza udahili . Na katika kazi ya ukarabati Mhe. katika Wilaya tuna uzoefu na kazi za ujenzi kupitia mfumo wa Force account, tutasaidia kuhakikisha kazi inafanyika kwa ubora ili thamani ya pesa ionekane," ameongeza Mhe. Kaegele.

Mhe. Jumanne Sagini, Mbunge wa Butiama ameipongeza Wizara ya Elimu kwa kutoa fedha kukiendeleza Chuo cha MJNUAT kuhakikisha sasa kinakwenda kuanza kutoa mafunzo, kuunda Baraza, kuteua Mwenyekiti na Mkuu wa Chuo.

"Napongeza pia mtazamo wa Wizara kuhusu mafunzo kuhakikisha yanajenga ujuzi. Hii inaashiria kuwa vijana wakitoka hapo MJNUAT wataweza kujiajiri katika kilimo," ameongeza Mhe. Sagini.

Kwa upande wake Kaimu Makamu Mkuu wa chuo cha MJNUAT, Prof. Lesakit Mellau amesema chuo hicho kinaendeshwa kwa usajili wa muda 'provisional registration license' na kwamba kilianza rasmi Machi 2015 baada ya Rais wa Awamu ya Nne, Dkt. Jakaya Kikwete kuteua viongozi.

Amesema kuwa tayari wameshaandaa mitaala 29 ikiwemo 20 ya Shahada ya Awali na 9 ya Diploma na kuongeza kuwa udahili unaotarajia kuanza baadae mwaka huu utaanza na wanafunzi 400.

Mkazo Elimu ya Malezi >

# Prof. Mkenda aitaka ADEM kuboresha Elimu ya Malezi kwa Walimu



Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Adolf Mkenda ameitaka Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu (ADEM) kulipa uzito wa kutosha suala la Malezi katika mafunzo wanayotoa.

Waziri Mkenda amesema hayo Wilayani Bagamoyo Mkoani Pwani alipotembelea Taasisi hiyo kuangalia utekelezaji wa majukumu yake ambapo amesema walimu wana nafasi kubwa katika malezi ya watoto kwa kuwa watoto wanatumia muda mrefu wakiwa shule hivyo mafunzo ya malezi yakitolewa yatasaidia sana wawapo katika mazingira ya kazi.

"Katika suala la Uongozi na Usimamizi wa Shule, ADEM iangalie namna ya kufundisha masuala ya malezi kwa walimu ili itusaidie kujua tunafanyaje kuwa na taratibu ambazo zitawasaidia walimu kwenye masuala ya malezi. Viongozi wa dini wanafanya hivyo lakini walimu wana nafasi kubwa zaidi," amesema Mkenda.

Amesema Taifa lolote ili liendelee ni lazima liheshimu elimu na katika kuheshimu elimu ni lazima kuheshimu mwalimu hivyo inasikitisha kuona baadhi ya walimu ambao wanawafanyia ukatili kwa watoto na kushusha hadhi ya mwalimu akitolea mfano tukio la hivi karibuni la mwalimu kumfanyia ukatili mwanafunzi kwa kumchapa viboko kupitiliza.

Aidha Waziri Mkenda amesema wakati Serikali ikiendelea kuleta fedha kwa ajili ya kuboresha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji, tujenge mkakati wa kutumia wahitimu katika kuboresha shule zetu kwa kuwa mahitaji yanaongezeka, pia ADEM iwafundishe Walimu na Viongozi wa elimu juu ya utafutaji wa rasilimali ikiwemo ushirikishwaji wa jamii ili kuendelea kuboresha mazingira ya utoaji wa elimu nchini.

"Tumesema hakuna michango ya lazima lakini tunahimiza michango ya hiyari. Baada ya kuwa Mbunge kampeni yangu ya kwanza ilikuwa kujenga vyoo bora shuleni na nikaandika barua nyumba zote za ibaada kwamba mwisho wa mwaka watu wanapokuja watembelee shule walizosoma kuona kama kuna kitu wanaweza kusaidia na imekua na matokeo chanya," ameongeza Prof. Mkenda.

Waziri Mkenda ameongeza kuwa Menejimenti ya mitihani ni nzuri na kupongeza Baraza la Mitihani la Taifa, Walimu na Wasimamizi kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Pamoja na kazi nzuri inayofanyika Mhe. Mkenda ameilekeza ADEM kufundisha walimu miiko na maadili ya Uongozi ili wachache wanaoshiriki katika udanganyifu wajue kukiuka miiko na maadili ya kiutumishi katika usimamizi wa mitihani kunaweza kusababisha wanafunzi kufaulu kwa udanganyifu.

Naye Mtendaji Mkuu wa ADEM, Dkt. Siston Masanja Mgullah amesema wamekuwa washauri wa nchi jirani katika kuanzisha Taasisi ya Uongozi na Usimamizi wa Elimu akitolea mfano nchi za Afrika ya Kusini, Angola, Msumbiji, Malawi ambapo matokeo ya ushauri huo yamekuwa mazuri.

Mtendaji mkuu huyo amemshukuru Rais Samia kwa kuwapatia fedha kwa ajili ya ujenzi wa Kampasi ya Mbeya na kuendelea kutenga fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi wa jengo la mihadhara Kampasi ya Bagamoyo lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,000.



Mageuzi Makubwa katika Elimu >



# Tunaelekea kufanya Mageuzi katika Elimu, Mageuzi yaanzie kwenye utendaji wetu

## ■ Tufanye kazi kwa weledi, ubunifu na kutoa huduma kwa ubora

Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Profesa Carolyne Nombo amewataka watumishi wa Wizara hiyo kufanya kazi kwa umahiri, weledi na ubunifu ili malengo ya sekta ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yaweze kufikiwa.

Prof. Nombo ametoa wito huo jijini Dodoma wakati wa mapokezi yake na Naibu Katibu Mkuu Dkt. Franklin Rwezimula baada ya kuteuliwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambapo amesema Wizara hiyo imepewa majukumu makubwa ya kuhakikisha elimu inayotolewa kwa Watanzania inakuwa bora na kuimarisha Sekta ya Sayansi na Teknolojia.

Ameongeza hivi sasa Wizara ipo katika hatua za mwisho za kuhuisha Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 na Mitaala, huku akisisitiza kuwa si Tanzania pekee inayofanya mageuzi hayo bali Dunia nzima ipo katika kufanya mageuzi ya elimu.

"Mageuzi katika utendaji kwa kufanya kazi kwa weledi, umahiri, ubunifu na uwazi ni muhimu ili kufikia yale mageuzi tunayoyatamani katika sekta ya elimu," amesisitiza Katibu Mkuu.

Prof. Nombo amemshukuru Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuwaamini na kumpa nafasi katika utumishi huo.

Aidha amewashukuru Makatibu Wakuu waliotangulia kwa kuweka misingi imara katika kuelekea mageuzi nchini.

Naye Naibu Katibu Mkuu, Dkt. Franklin Rwezimula amemshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kumuamini na kumpa nafasi ya kutumikia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, huku akiahidi kutoa ushirikiano kwa watumishi ili kuendelea kuboresha sekta ya elimu.

[28/02, 15:00] Ipyana: Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Ofisi ya Rais TAMISEMI kwa kushirikiana na Benki ya Dunia kupitia Mradi wa Kuimarisha Ubora wa Elimu ya Sekondari (SEQUIP) inaendesha mafunzo ya siku tano kwa walimu wa shule za sekondari za umma wanaofundisha masomo ya Sayansi na Hisabati.

Katika Mwaka wa Fedha 2022/23 Mradi unatarajia kutoa mafunzo kwa walimu 20,000 wa Sayansi na Hisabati na utaendelea kutoa mafunzo haya katika mwaka ujao wa fedha ili kukamilisha kutoa mafunzo kwa walimu wote wa shule za sekondari za umma wanaofundisha masomo ya Sayansi na Hisabati.

Mpaka sasa mafunzo hayo yameshatolewa kwa zaidi ya walimu 8,000 kutoka mikoa ya Mwanza, Geita, Mara, Morogoro, Pwani, Dodoma, Singida na Tabora.



NUKUU > **TUTAJIELEKEZA KATIKA KUFANYA MAPITIO YA SERA YA ELIMU NA MAFUNZO YA MWAKA 2014 NA KUFANYA MAREKEBISHO KWENYE MITAALA ILIYOPO ILI IELEKEZWE KWENYE KUTOA ELIMU UJUZI KULINGANA NA MAZINGIRA YA NCHI NA SOKO LA AJIRA**

***– Mhe. Samia Suluhu Hassan,***
***Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania***
***Bungeni - April, 2021***

# Anuani za Taasisi zilizo chini ya Wizara

Katibu Mtendaji,
**Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU),**
Jengo la Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia,
S.L.P 6562,
7 Mtaa wa Magogoni,
11479 DAR ES SALAAM.
Simu: +255 22 2113694, 2113691
Barua Pepe: es@tcu.go.tz

Mkurugenzi Mtendaji,
**Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB),**
HESLB House, 1 Mtaa wa Kilimo -TAZARA,
Barabara ya Mandela,
P.O. Box 76068,
15471 DAR ES SALAAM.
Simu: +255 736 665 533/ 739 665 533
Baruapepe: ed@heslb.go.tz

Katibu mtendaji,
**Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA),**
Eneo la Viwanda Mikocheni,
Barabara ya Bagamoyo,
S.L.P 2624 au 32019,
14112 DAR ES SALAAM.
Simu: +255 22 2700493-6/9 na 22 2772423
Barua Pepe: esnecta@necta.go.tz

Mtendaji Mkuu,
**Baraza la Taifala Elimu ya Ufundi (NACTE),**
S.L.P 7109, DAR ES SALAAM.
Simu:
Barua Pepe: info@nacte.go.tz

Mtendaji Mkuu,
**Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu (ADEM),**
Nunge Street, Old Catholic Church Road,
S.L.P 71, BAGAMOYO, PWANI.
Simu: +255 23 244 0216
Barua Pepe: adem@adem.ac.tz

Mkurugenzi Mkuu,
**Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH),**
Barabara ya Ali Hassan Mwinyi,
S.L.P. 4302,
14113 Kijitonyama,
DAR ES SALAAM.
Simu: +255 (022) 2771358/ 2774023/ 2700749
Baruapepe: dg@costech.or.tz

Mkurugenzi Mkuu,
**Taasisi ya Elimu Tanzania (TET),**
Plot 132, Barabara ya Ali Hassan Mwinyi
S.L.P. 35094, DAR ES SALAAM.
Simu: +255 0735 041168
Barua Pepe: director.general@tie.go.tz

Mkurugenzi Mkuu,
**Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA),**
S.L.P 34578,
Mikocheni B, Bima Road,
DAR ES SALAAM.
Simu:
Barua Pepe: info@tea.or.tz
dg@tea.or.tz

Mkurugenzi Mkuu
**VETA Makao Makuu,**
Plot No. 18, Central Business Park (CBP)
Barabara ya VETA,
S.L.P 802,
26 DODOMA.
Simu: +255 26 2963661
Baruapepe: info@veta.go.tz

Mtendaji Mkuu,
**Tume ya nguvu za Atomic Tanzania (TAEC)**
S.L.P 743,
23114 Engutoto, Block J, Plot No 216,
ARUSHA
Simu: +255 272 9700054
Barua Pepe:dg@taec.go.tz

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM),**
Kampasi ya Mwalimu Julius Nyerere Mlimani,
S.L.P. 35091, Mtaa wa Chuo Kikuu
16103 Dar es Salaam
Simu: +255222410700
Baruapepe: vc@udsm.ac.tz

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Ardhi University (ARU),**
Plot No. 3, Observation Hill Blok L,
University Road,
P.O. Box 35176, DAR ES SALAAM.
Simu: +255 738 357 310-12
Baruapepe: aru@aru.ac.tz

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi, Muhimbili (MUHAS),**
9 Barabara ya Umoja wa Mataifa,
Upanga Magharibi,
S.L.P. 65001,
11103 DAR ES SALAAM.
Simu: +255 22 2150302-6
Baruapepe: vc@muhas.ac.tz

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu cha Sokoine (SUA),**
S.L.P 3000,
Barabara ya Edward Moringe, Mtaa wa Kilimo,
01 MOROGORO
Simu: +255 23 260511-4
Barua Pepe: sua@sua.ac.tz

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu Mzumbe (MU),**
S.L.P 1, MOROGORO
Simu:
Barua Pepe: mu@mzumbe.ac.tz
info@mzumbe.ac.tz

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM),**
S.L.P 259,
Mtaa wa Benjamin Mkapa,
Jengo la Benjamin Mkapa,
41107 DODOMA.
Simu: +255 26 2310001/2/3
Barua Pepe: vc@udom.ac.tz
relations@udom.ac.tz

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu Huria Tanzania (OUT),**
S.L.P. 23409,
14110 Open University Road,
Kinondoni Municipality,
DAR ES SALAAM
Simu: +255 22 2668820/ 2668992
Baruapepe: vc@out.ac.tz

RASI wa Chuo,
**Chuo Kikuu kishiriki cha Elimu Dar es Salaam (DUCE),**
Taifa Road Next to Benjamin Willium,
S.L.P. 2329,
15105 DAR ES SALAAM.
Simu: +255 22 2850975
Barua Pepe: principal@duce.ac.tz
dpacademic@duce.ac.tz

Mkuu wa Chuo,
**Chuo cha Ushirika Moshi,**
06 Barabara ya Sokoine Moshi,
S.L.P 474
KILIMANJARO
Simu: +255 272 751 833
Barua Pepe: info@mocu.ac.tz

Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kushiriki Cha Elimu Mkwawa (MUCE),**
Mtaa wa Mkwawa Chuo,
S.L.P. 2513,
51111 IRINGA CBD.
Simu: +255 26 2702 751
Baruapepe: principal@muce.ac.tz

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu Cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST),**
S.L.P. 131,
Barabara ya 01 MUST,
01 MBEYA.
Simu: +255(0)25 2957542/4
Barua pepe: vc@mustnet.

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Taasisi ya Afrika ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela (NMIST),**
Kampasi ya Tengeru, Barabara ya Nelson Mandela,
S.L.P. 447,
23301 TENGERU, ARUSHA
Simu +255 272970001
Baruapepe: vc@nm-aist.ac.tz

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu cha Mwalimu Julius Kambarage Nyerere,**
S.L.P 976, Butiama, MARA
Simu:
Barua Pepe: info@mjnuat.ac.tz

Mkurugenzi
**Bodi ya Huduma za Maktaba (TLSB),**
27 Mtaa wa Bibi Titi Mohamed,
S.L.P 9283
DAR ES SALAAM
Simu: +255 22 2150048/9
Barua Pepe: info@tlsb.go.tz

Katibu Mtendaji,
**Tume ya Taifa ya UNESCO,**
7 Magogoni Street,
P. O. Box 20384,
11479 DAR ES SALAAM
Simu: +255 22 2126598/ 22 2134292
Baruapepe: info@natcom.go.tz

Mkurugenzi,
**Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima (TEWW)**
23 Mtaa wa Bibi Titi Mohammed,
S.L.P. 20679,
11103 DAR ES SALAAM
Simu:
Baruapepe: info@iae.ac.tz

Mkuu wa Chuo,
**Chuo cha Ufundi Arusha (ATC),**
Junction of Moshi-Arusha and Nairobi Roads,
P.O. Box 296,
23105 ARUSHA.
Simu: +255 (0) 27-297 0056
Baruapepe: rector@atc.ac.tz/pro@atc.ac.tz

Mkurugenzi,
**Kituo cha Maendeleo Dakawa,**
S.L.P 1733,
MOROGORO.

Mkuu wa Chuo,
**Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT),**
Kona ya Bibi Titi na Barabara ya Morogoro
S.L.P 2958
11104 DAR ES SALAAM
Simu:
Barua Pepe: principal@dit.ac.tz

Mkuu wa Chuo,
**Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere (MNMA),**
30 Barabara ya Kibada,
S.L.P 9193,
17107 Kigamboni,
DAR ES SALAAM.
Simu:
Baruapepe: rector@mnma.ac.tz